BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Sita – Tarehe 06 Mei, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

37. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Katika kufanikisha jitihada za kuimarisha Uchumi wa Buluu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imehamasisha wawekezaji kuja kuweka Zanzibar.

(a) Je, kuna jitihada zozote zinazofanywa au mpango ili kuwahamasisha wawekezaji wa ndani kuekeza Zanzibar.

(b) Je, ni mikakati gani imewekwa katika kuimarisha viwanda vinavyotumia mazao ya uvuvi, kilimo na mifugo kwa wawekezaji wa ndani.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kulinda soko kwa viwanda vyenye kutumia malighafi za ndani.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

54. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mkoa wa Kaskazini Pemba hadi sasa hakuna eneo maalum la mnada wa ng'ombe na mbuzi wala gulio maalum kwa ajili ya bidhaa mbali mbali zinazozalishwa ndani ya Mkoa huo, jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu kwa wakulima na wafugaji.

(a) Je, ni lini Serikali itawatengea eneo maalum kwa ajili ya shughuli hizo.

(b) Je, ni upi muongozo wa Serikali kuhusu watu binafsi wenye nia ya kuanzisha maeneo maalum ya mnada wa ng'ombe na mbuzi pamoja na magulio maalum ya kuendesha biashara hizo.

Wizara ya Afya:

11. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi inastahili pongezi kwa kuziimarisha vizuri huduma za afya. Hata hivyo, shehia ya Wambaa haina kituo cha afya na ukizingatia wananchi hao wanapata tabu sana.

(a) Je, ni lini wananchi hawa watapatiwa kituo cha afya.

(b) Je ni lini tutakwenda pamoja ili uone kadhia wanayoipata wananchi wa shehia ya Wambaa.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

40. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi kubwa katika kuwaletea maendeleo wananchi wake, kurahisisha mawasiliano na kuweka miundombinu imara, ingawaje bado kuna changamoto kwa baadhi ya maeneo.

(a) Je, ni lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano katika shehia za Msuka jimbo la Konde ili kuwaondolea usumbufu wanaoendelea kuupata wananchi wa maeneo hayo.

(b) Kwa kuwa wananchi hao wamesubiria muda mrefu na kuvumilia changamoto hiyo. Je, ni lini Wizara itaenda kuwapa moyo wananchi hao na kuwajengea matumaini.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

18. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika hotuba zake Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi amelitaka Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kuwapatia nguzo wananchi wote wanaotaka kuungiwa umeme katika maeneo

yao bila ya malipo yoyote. Gharama ya nguzo hizo zitabebwa na Serikali kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi hasa wanaoishi vijijini.

(a) Je, Wizara inafahamu kwamba wananchi wanapokwenda katika Shirika hili kwa lengo la kupatiwa huduma hii hutakiwa kulipia gharama ya nguzo kwa fedha nyingi sana.

(b) Je, Wizara haioni kwamba kutenda hivyo ni kwenda kinyume na agizo la Mheshimiwa Rais hasa tukizingatia kuwa wananchi wetu wanaamini kuwa maagizo ya Mheshimiwa Rais huwa ni amri.

(c) Je, Wizara inawaambia nini wananchi wetu ambao hawana uwezo wa kununua nguzo hizo kupitia Shirika la Umeme Zanzibar.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

6. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Eneo la viwanja vya michezo vya Mnazimmoja limekuwepo kwa miaka mingi na kutoa mchango mkubwa katika michezo pamoja na kuzalisha vipaji vya michezo mbali mbali. Hata hivyo, muda umefika sasa wa viwanja hivyo kutumika kisasa zaidi.

(a) Je, kwa nini Serikali haitafuti wawekezaji watakaoweka huduma mbali mbali kama vile vituo vya huduma za fedha, mawasiliano na vyenginevyo ili kuleta mvuto na tija katika eneo hilo.

(b) Je, Serikali imeweka mpango wowote wa kuongeza thamani ya maeneo yale ili ipatikane tija zaidi.

70. MHESHIMIWA ABDALLA ABAS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mbali na michezo mengine inayochezwa hapa Zanzibar, mchezo wa riadha ni mchezo unaopendwa hapa visiwani hasa mnamo mwaka 1970 – 1980.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazoufanya mchezo huo

watu wasiupende kama ilivyo miaka ya nyuma.

(b) Je, ni vilabu vingapi vipo ndani ya Mikoa ya Zanzibar.

(c) Kama vilabu vya riadha havijaundwa katika Mikoa yetu ni lini vitaundwa.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

66. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar ilipanga kuzalisha miche bora na salama ya migomba, mhogo na viazi vitamu kwa njia ya chupa (tissue culture) na kuisambaza kwa wakulima.

(a) Je, Wizara kupitia taasisi hiyo imetekeleza suala hilo kwa kiasi gani.

(b) Je, ni wakulima wangapi wamepata mgao huo.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

29. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba na ya Nane zimesisitiza utalii kwa wote lakini uhalisia bado azma hiyo haijafikia kwa kiwango kizuri.

Je, Serikali kupitia Wizara yako ina mkakati au mpango gani wa kuweza kufanikisha azma hiyo.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

24. MHESHIMIWA HABIBU ALI MUHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alifanya mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri katika kuimarisha utendaji kazi wa Serikali na kukuteuwa wewe kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Je, ni kwa kiasi gani utasimamia maslahi ya ongezeko la mishahara ya walimu, jambo ambalo mtangulizi wako hakulifanyia kazi suala hilo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
06 Mei, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA